# MASENO SCHOOL

**Jina.................................................Nambari ya Mtahiniwa......................**

**Sahihi ya Mtahiniwa...........................................Tarehe..........................**

# SHULE YA KITAIFA YA MASENO

## MTIHANI WA MWIGO

## KISWAHILI

## 102/3

## Karatasi ya 3

## FASIHI

## Muda: Saa $2^{1}/_{2}$

102/3-Fasihi- P3

Jumatano 17/07/2019

Muda: 8:00-10:30 asubuhi

**Maagizo**

a) Jibu maswali manne pekee.
b) Swali la kwanza ni la **lazima.**
c) Maswali mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:
d) Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
e) Usijibu maswali mawili katika sehemu moja.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
g) Majibu yote yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
h) Karatasi hii ina kurasa **8** zilizopigwa chapa.
i) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

| Swali | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama | | | | | | | | | |

MASENO SCHOOL

## SEHEMU A: HADITHI FUPI

1. **Lazima**
    a) Ni karne ya ishirini na moja lakini bado mtoto mvulana anaishi maisha ya kutatarisha.Thibitisha kauli hii ukirejelea hadithi zifuatazo:
        i) Mapenzi ya Kifaurongo (alama 4)
        ii) Ndoto ya Mashaka (alama 4)
        iii) Mtihani wa Maisha (alama 4)

    **SHIBE INATUMALIZA na Salma Omar Hamad**

    ‘’Sijali lawama mnonilaumu’’

    b) Eleza namna wahusika wafuatao hawakujali lawama kwa mujibu wa dondoo:

        i) DJ (alama 4)

        ii) Mzee Mambo (alama 4)

## SEHEMU YA B: RIWAYA

**Assumpta Matei:***Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au 3.*

2. “… maisha yalitubadilikia mara tu baada ya kuondoka kwako. Tuliandamwa na msiba baada ya mwingine.”
    a) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)
    b) Huko ukitoa hoja sita, eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
    c) Eleza misiba yoyote kumi inayomwandama msemaji wa maneno haya. (alama 10)
3. “Wanawake ni viumbe wa kushangaza sana…”
    a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
    b) Huku ukitoa hoja nane kutoka kwenye riwaya, dhihirisha kuwa wanawake ni viumbe wa kushangaza. (alama 8)

c)“Sasa ninaamini usemi wa Tila wa kila mara kuwa haifai kucheza na uwezo wa vijana, wao ni kama nanga. Huweza kuzamisha na kuongoa merikebu”

Huku ukitoa hoja nane, eleza namna vijana wanazamisha merikebu inayorejelewa. (alama 8)

**SEHEMU YA C :TAMTHILIA**
**Pauline Kea.:** *Kigogo*
***Jibu swali la 4 au 5***

4. "…Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha kichwa!Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana…"
   a) Fafanua sifa sita za msemaji (alama 6)
   b) Changanua maudhui yanayojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 14)

5. ''Tunahitaji kuandika historia yetu upya."
   i. Tambua visa sita vinavyothibitisha kutoandikwa vizuri kwa historia ya Sagamoyo. (alama 6)
   ii. Eleza mikakati minne iliyotumiwa kuandika upya historia ya warejelewa. (alama 4)
   iii. Mwandish amewaumba wanawake na kuwaumbua wanaume.Tetea kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya kigogo.( alama 10).

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
***Jibu swali 6 au 7***

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

**Kutegea kazi**
Twakimbilia ndani
Eti kutafuta kazi
Kazi kuepuka ukame
Ambao mengi umetuletea:
Kiu isokwisha
Na damu kugandisha
Kwa ukiwa unaotisha
Pia ngozi kunyausha
Hata tumbo kusongolesha

Ngo!Ngo!Ngo!Tunabisha
Kimya
Lango limekomewa komo!
Madirisha yamesindikwa ndi!
Hakuna wenyewe?...Hakuna kazi!

Tutaingia wapende wasipende
Naam!Miale ya hisi zetu inapenya
Tunaona jumbani wamejaa Watende
Wenye haiba na mabwebwe tele
Nyuso mithili viwele

Mikogo belebele
Lakini mbona hawafungui?

Mnunurisho unapenya
…sasa tunaona
Aliyeshika  mwananchi
Penye fumbo la maneno
Mwenzake hana neno
Anafuma mshono
Pembeni mwingine anasimulia
Vitimbi vya Jumamosi
Naye wa vyombo masikioni
Anayumba kwa mdundo…ya kizazi kipya
Halafu viti…kuna viti bila watu
Kumbe viti huvishwa makoti?
Kwa mbali kuna kundi

Soga linachemka kama tindi
Lalama zao zafoka kama jini
Mara mshahara duni
Maslahi wametuhini
Kazi nayo ya majinuni
Kompyuta haina fani
Lakini mbona miili yao imetuna?
Mbona wamekaa wananena?
Mbona kompyuta yacheza karata?

Enyi mlio ndani
Msisahau ubaharia…
Wewe…ninyi…mngejua!
Mngelikaza si kulegeza misuli
Kuvuvisha si kuviza ari
Nyote mngependa kazi si kutegea kazi
Kwani ni tatizo kujituma?
Eti bila chai mambo hukwama?
Tuzinduke kazi tuipe udole
Kipaumbele tuichape hadi kilele
Njuga tuivalie kuondoa uchochole
Matone ya jasho yawe chemchemi ya ajira tele
Nacho kipato kinawiri kama mchele
Uzembe ni ndwele,tusiupe simile.

Maswali

a) Dhihirisha kuwa kichwa cha shairi hili kinafaa. (alama 2)
b) Eleza toni inayojitokeza katika  shairi hili.        (alama 2)
c) Tambua nafsineni katika shairi hili.                 (alama 2)
d) Huku ukitoa hoja nane, eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. (alama 8)
e) Tambua mbinu nne za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)

f) Eleza maana za vifungu vya maneno vifuatavyo: (alama 2)

i. Bila chai mambo hukwama

ii. kazi tuipe udole

7. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali

**SHAIRI A:**

Siku moja itafika, katika hii dunia
Itapozuka *fanaka*, kupotea kwa balia
Haki itakaposhika, batili kuangamia

Uhuru utakapodumu, sio ule wa bandia
'Tasitawi mwanadamu, kila atojifanyia
Na hilo jambo karibu, haitimu myaka mia

Utakwenda udhalumu, katu hautorejea
Itatuishaia tabu, waliotusukumia
yatasibu*matulubu*, yale tunayowania

Na nyanyaso litapita, kizazi kipya kuingia
Na uasawa kitaleta, tena kitashikilia
Na machozi tutafuta, maisha mapya huria

Dunia 'tapoamka, itakapoona njia
Hizi shida taondoka, tutaumana kwa nia
Hili jambo la hakika, tarehe meshatwambia
*(Said A. Mohamed, Maisha Mapya 'Sikate Tamaa)*

**SHAIRI B:**

Leo alasiri
Ndoto zangu
Ziliona picha
Picha ya kupendeza
Kama jua angavu
    Jua la utu
    Lilianza kung'aa
    Na kupamba anga
    Kwa mwangwa mtamu
    Nalo wingu la mashaka
    Likaanza *kutanduka*
    Hatimaye likafutika

Leo alasiri
Ndoto zangu

Ziliona picha
Picha ya kupendeza
Kama upinde-wa-mvua
    Mti wa haki
    Ulianza kuimarika
    Na *kufariji* nyoyo
    Kwa kivuli kizito
    Nao mnga wa dhuluma
    Ukaanza kukauka
    Hatimaye ukaanguka
*(Kithaka Wa Mberia, Pacha La Picha, Mchezo Wa Karata)*

**MASWALI**

a. Fafanua matumaini ya washairi katika mashairi haya (alama 4)
b. Fafanua taswira mbili zainazojitokeza katika shairi B (alama 2)
c. Andika ubeti wa pili wa shairi B katika lugha nathari. (alama 4)
d. Taja na ufafanue sifa za kiarudhi zinazojitokeza katika shairi A. (alama 4)
e. Toa mifano miwili ya tashibihi katika shairi B. (alama 2)
f. Eleza maana ya maneno yafautayo kama yalivyotumiwa katika mashairi haya (alama 4)

I. fanaka-
II. matulubu -
III. kutanduka -
IV. kufariji -
V.

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale katika kitongoji cha Shwari, paliishi Sungura na Fisi. Sungura na Fisi walikuwa marafiki wa chanda na pete. walizama na kuibuka katika bahari mbalimbali za maisha. Marafiki hawa walizilea aila zao pamoja. Walifanya kazi kwa ujima mashambani na kushiriki pamoja vunoni. Mvua nayo ilinyesha msimu baada ya mwingine. Makonde yao yakanawiri na maghala yao yakaanza kulalamikia shibe. Pia walichunga mifugo wao pamoja.

Watoto wa Sungura na Fisi walicheza pamoja bila kujali tofauti zao za kimaumbile. Waliamka alfajiri na mapema kwenda kuwachunga mifugo ya wazazi wao. Kadiri siku zilisonga, ndivyo gundi iliyougandisha udugu kati ya familia hizi ilivyoendelea kunata.

Hata hivyo, siku za neema zilipisha shari. Mvua ilikataa katakata kukitembelea kijiji chao. Polepole, akiba ya chakula waliyokuwa wameiweka ikaanza kupungua. Mwishowe ikakauka kabisa.

Fisi alikesha kitandani kwa tafakuri kuu. Hali ya baadaye ya familia hizi mbili ilimsononesha. Alihofia kuwaona wanao wakigeuka magofu. Asubuhi moja baada ya yeye na familia yake kula mate usiku uliotangulia, alimwendea Sungura na kumtaka washauriane kuhusu mkakati wa kukabiliana na hali mbaya iliyowasibu.

Baada ya kutia na kutoa, wazo lilimjia Sungura. "Ndugu yangu, janga hili la njaa ni tokeo la hasira za mizimu. Mababu zetu walikosa nasi hatuna budi kuangukiwa na laana za mizimu. Jana usiku, mizimu ilinijia usingizini, iliniambia kuwa njia ya pekee ya kujiopoa na familia zetu ni kwa kuituliza kwa kuitolea kafara. Tukifanya hivyo, mvua itanyesha mara moja na tutaweza kuyanusuru maisha wa watoto wetu."

Kipaji cha fisi kilinawiri kwa furaha. Hata hivyo, tabasamu yake haikudumu. Alizama tena katika fikira. Baada ya kutafakari kwa muda, alimuuliza Sungura, "Ndugu yangu, mifugo wetu wote wamesalimishwa amri na ukame. Je, tutatoa wapi kafara?"

Sungura alijibu kwa huzuni, "Mizimu yenyewe haitaki mifugo wala nafaka. Inataka damu. Damu ya binadamu pekee ndiyo inayoweza kufuta dhambi za mababu zetu."

"Na binadamu mwenyewe watatoka wapi?" aliuliza Fisi.
"Hilo ndilo tatizo. Mizimu inataka tuwatoe sadaka mama zetu na vifunguamimba wetu. Leo usiku, wanataka kila mmoja wetu amuue mama yake na kumtoa kama sadaka kwenye mbuyu ulio karibu na mto." Sungura alisema.

Maneno ya Sungura yaliyafanya masikio ya Fisi kuvuma kwa uchungu wa fikira ya kumpoteza mamake. Alimpenda mamake kwa dhati. Aidha, alijua kuwa haikuhalisi binadamu kumua mwenzake. Hata hivyo, nafsi yake ilimnasihi kwamba alihitaji kufanya uamuzi wa dharura. Jioni hiyo, sime yake alifanya kazi. Alikata koo la mama yake mpenzi huku majonzi yakimtiririka. Aliuchoma mwili wa mamake pale mbuyuni huku akiimba:

*Enyi mizimu mtoao vipaji,*
*Nimewapeni roho ya kipenzi mama yangu,*
*Itumeni mvua kuineemesha ardhi.*

Fisi aliondoka huku akijituliza kuwa hata sungura naye amemchinja mama yake.

Usiku huo, mvua ya gharika ilinyesha. Mashamba ya Sungura na Fisi yakajaa chakula mara moja. Zizini, ng'ombe wakasika wakikoroma na ardhi ikavaa vazi la kijani kibichi. Wakati wote huo Sungura hakuonekana nyumbani. Fisi alidhani kwamba huzuni ya kumpoteza mama yake ilimlemea, hivyo akaamua kwenda mbuyuni kumtafuta. Hata kabla hajavuka kizingiti cha mlango, alikumbana ana kwa ana na mama yake Sungura. Malaika yalimsimama mwilini, mate yakamkauka kwa mshangao! 'Kumbe Sungura hakumtoa kafara mamake? Kumbe maneno yote ya Sungura yalikuwa ulaghai ili mimi Fisi nimtoe kafara mama yangu na kuiauni jamaa ya

Sungura!' moyo wa Fisi ulifungwa kwa fundo kubwa la chuki kwa Sungura. Huo ukawa mwisho wa urafiki wao.

**Maswali**

a) Dhihirisha kuwa ngano hii ni; (alama 3)

i. Ngano ya usuli

ii. Ngano ya kiayari

iii. Hurafa

b) Eleza sifa tano za ngano zinazojitokeza katika ngano hii. (alama 5)

c) Hii ngano ina mafunzo mbalimbali. Eleza yoyote manne. (alama 4)

d) Tambua shughuli zozote mbili za kiuchumi na mbili za kidini zinazojitokeza kwenye ngano hii. (alama 2)

e) Eleza namna tatu za kisasa ambazo unaweza kuhifadhi ngano za aina hizi. (alama 3).

f) Eleza sababu tatu za kurithisha ngano hii kwa vijana wa kisasa katika jamii. (alama 3)